

\*AMKA NA ALFALFA TANZANIA\*

MAJANI JAMII YA MIKUNDE!

Yafuatayo ni Majibu ya Maswali yaliyoulizwa na wafuatiliaji Wa Kilimo cha Alfalfa Tanzania.

Majibu haya yanaletwa na Ndugu Adam Ngamange (Mkurugenzi Wa Mtandao Wa Kijani Kibichi Tanzania), Dr Mary (Mtafiti Kibaha Kituo cha Utafiti) na Mkulima Maarufu Wa Majani Mkoani Pwani Ndugu Nuru Mohammed

#### UTANGULIZI

Kilimo Biashara cha Alfalfa Tanzania ni Kilimo Kamilifu (Comprehensive farming) yaani kilimo Shamba hadi Sokoni (From farm to fork), ni Kilimo kinachoangalia mzunguko mzima Wa kuongeza thamani kupitia mnyororo Wa uzalishaji. Kilimo hichi kitawahusisha watafiti katika ngazi zote kuanzia Shamba hadi Dukani.

#### SWALI LA KWANZA

Ni zao Zuri Kibiashara?

Yes ni zao zuri mno!

Kibiashara, Kiafya na Kimazingira hususani kwa Tanzania ya sasa kwasababu;

Alfalfa nini?

Ni mmea unaota mithili ya vichaka, wenye kutenga na kupendeza kwa kutazama, ni mmea wenyekustawai katika hali ya kitropical yenye mvua kuanzia mm500 usawa Wa bahari. Kwa ufupi zaidi ya 75% ya Tanzania mmea huu ustawi kwa ubora wake lakini ukanda Wa Kijani Tanzania (Ukanda Wa Pwani, Mashariki na Kusini ni zaidi ya kawaida)

#### KIBIASHARA

Alfalfa linawateja Wa aina mbalimbali hususani wakati huu gharama za vyakula na madawa kwa wafugaji zipo juu, alfalfa ni zao linalotumika kwa chakula na lishe tiba.

Alfalfa ni kwa ajili ya Mifugo yote kuanzia Sungura, Farasi, Ng'ombe, Mbuzi Kuku, Nguruwe kwa wafugaji hii ni Neema kubwa kule Arusha na Iringa wanajua sana kuhusu hii kitu. Wataalamu na makampuni ya vyakula vya wanyama hii ni chakula mbadala ya madawa

#### ALFA NA UDONGO!

Alfalfa ni chakula cha udongo na mimea mingine utengeneza nitrogen kwa utaratibu kisayansi wanaita Nitrogen Fixation. Madini ya nitrogen yanahitajika mno kujenga ustawi Wa mimea kama ilivyo mikunde mingine kama maharagwe.

Alfalfa ulinda mmong'onyoko Wa ardhi. Mazingira ya mmea huu ni kuunganisha udongo na kufanya udongo kushikamana.

#### Asali ya Alfalfa (Alfalfa Honey)

Moja ya asali ghali duniani na ya alfalfa inayopatikana kutokana na Maua ya alfalfa ingia kwenye mitandao kama ya Americans online utaona vipi hii asali ilivyo ghali

Alfalfa ni Chakula lishe kwa binadamu. Kachumbali ya alfalfa ni nadra mno kukuta kwa watu Wa hali ya chini, kumbuka majani na Maua ya alfalfa yana protein isiopungua asilimia 25, yana vitamini A,B,C,K,H bila kusahau madini kwa wingi.

#### MBEGU ZA ALFALFA

Baada ya miaka NNE ya hii mimea hukomaza Mbegu na hizi Mbegu ni dawa sana kwa ajili ya kuongeza CD4

Hili zao la alfalfa ni bora kifedha, kiafya na kimazingira. Usikose kufuatalia kwa ukaribu hesabati ya alfalfa kiuchumi

#### SWALI LA PILI

Linavunwa Mara ngapi?

Mmea Wa alfa ukipandwa kwa kufuata ushauri Wa wataalamu linachukua miezi mitatu kuvunwa kwa mvuno Wa kwanza na kila siku 45 hadi 60 utakuwa unavuna alfalfa kwa miaka minne hadi 8 mfululizo.

Hili zao linahitaji sana maji, maji kwa wingi ndivyo mavuno kwa wingi na kwa muda mfupi mfupi.

Kwa Leo naomba niishie hapo subiri kwa hamu kubwa hesabati ya Alfa, wapi Alfa inalimwa kwa wingi Duniani, Afrika, Afrika ya Mashariki na Tanzania.

Unaweza pia kujiorodhesha kwa mafunzo ya Alfa Kibiashara yatakayofanyika KIBAHA ( Nadharia na vitendo kwenye kituo cha kilimo cha majani vikuga)

Tupia jina na namba yako 0783038760

Alfalfa ni Zao Dume ya Mazao Mengine na Adam Ngamange